

## Fentanyl ya Ndani ya mapua

Fentanyl ya ndani ya mapua ni dawa inayofanya kazi kwa haraka na ufanisi ya kudhibiti maumivu. Inatolewa kwa kunyunyizia dawa ndani ya pua lako. Ni chaguo bora wakati hatuna dawa ya sindano ya mshipa.

Tunajua umuhimu wa mpango wa kudhibiti maumivu wa kila mtu. Tunapanga kubadilisha uwe unatumia dawa ya kudhibiti maumivu ya sindano (kitulizaji) inayokufaa zaidi wakati utapata dawa ya sindano. Hatua muhimu katika kudhibiti tatizo la maumivu ni kutibu maumivu mapema. Dawa hii inakusaidia kuanza mapema kutibu maumivu yako ili yasikithiri sana. Hii imedhihirisha kupunguza hitaji la kulazwa hospitalini.

Fentanyl ya ndani ya mapua ni dawa ya kawaida sana tunayotumia kutibu aina zote za maumivu, kama vile, mifupa iliyovunjika, kuchomeka na majeraha mengine. Inapendekezwa kama dawa ya kawaida nchini kwa utulizaji wa haraka wa maumivu ya ugonjwa ya selimundu.

Ni dawa inayofanya kazi kwa haraka na ni rahisi kutumia. Tunaweza kupendekeza dozi kulingana na mahitaji ya kila mtu. Inafanya kazi ndani ya dakika chache. Umri na uzani wa mtoto wako hutumiwa kubaini dozi salama na ya ufanisi.

Kama ilivyo na dawa zingine za kutuliza maumivu, fentanyl inaweza kusababisha athari ambazo kwa kawaida huwa za muda mfupi na huisha. Hizi ni pamoja na:

- kusinzia
- kizunguzungu
- kichefuchefu

Fentanyl ya kunyunyizia ndani ya mapua haina chungu. Nusu ya dozi huwekwa kwenye pua moja na dozi hio nyingine kwenye pua la pili Unachohitaji kufanya ni kubaki tuli na upumue kama kawaida.

Lengo letu ni kutoa huduma bora iwezekanavyo ili kukusaidia kudhibiti maumivu yako mapema.

## Marejeleo

Shirika la Marekani la Madaktari wa Huduma za Dharura (2023, Juni 22)). Jinsi ya kudhibiti ugonjwa wa selimundu katika Idara ya Dharura. <https://www.acep.org/patient-care/sickle-cell/>

Brandow, A.M., Carroll, C.P., Creary, S., Edwards-Elliott, R., Glassberg, J., Hurley, R.W., Kutlar, A., Seisa, M., Stinson, J., Strouse, J.J., Yusuf, F., Zempsky, W., & Lange, E. (2020). Mwongozo wa Shirika la Marekani la Magonjwa ya Damu wa 2020 kwa ugonjwa wa selimundu: Udhibiti wa maumivu kali na ya kudumu. *Blood Advances*, 4(12), 2656-2701. <https://doi.org/10.1182/bloodadvances.2020001851>

Kavanaugh, P.L., Sprinz, P.G., Wolfgang, T.L., Killius, K., Champigny, M., Sobota, A., Dorfman, D., Barry, K., Miner, R., & Moses, J.M. (2015). Kuboresha udhibiti wa matukio yanayotokana na selimundu ya kuzuia mzunguko wa damu katika chumba cha dharura cha watoto. *Pediatrics*, 136(4), e1016-e1025. <https://doi.org/10.1542/peds.2014-3470>

Puri, L., Nottage, K.A., Hankins, J.S., & Angheliescu, D.L. (2018). Udhibiti wa hali ya juu wa maumivu yanayotokana na selimundu ya kuzuia mzunguko wa damu katika wagonjwa wa selimundu. *Pediatric Drugs*, 20, 29-42. <https://doi.org/10.1007/s40272-017-0263-z>

Rees, C.A., Brousseau, D.C., Ahmad, F.A., Bennett, J., Bhatt, S., Bogie, A., Brown, K.M., Casper, T.C., Chapman, L.L., Chumpitazi, C.E., Cohen, D.M., Dampier, C., Ellison, A.M., Grasemann, H., Hatabah, D., Hickey, R.W., Hsu, L.L., Bakshi, N., Leibovich, S., ...Morris, C.R. (2023). Fentanyl ya ndani ya mapua na kuruhusiwa kuondoka chumba cha dharura kwa watoto walio na ugonjwa wa selimundu na maumivu yanayotokana na selimundu ya kuzuia mzunguko wa damu: Mtazamo wa vituo vingi wa dawa za dharura za watoto. *Jarida la Magonjwa ya Damu la Marekani*, 98(4), 620-627. <https://doi.org/10.1002/ajh.26837>